JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI

Ofisi: Ubungo
Simu: +255 22 2213701,
Barua pepe: rector@nit.ac.tz
Tovuti: www.nit.ac.tz

P.O. Box 705
DAR ES SALAAM
TANZANIA

# TAARIFA KWA UMMA

## KANUSHO JUU YA TANGAZO LA UWEPO WA MAFUNZO YA UDEREVA MAHIRI WA MASAFA MAREFU *TRANSIT DRIVERS*

*Dar es salaam.*
*Jumatano, Julai 1, 2026*

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimebaini kuwapo kwa taarifa inayosambazwa katika mitandao ya kijamii inayohusu madai ya kuwapatia ajira Madereva mahiri wa masafa marefu ndani na nje ya nchi wa mabasi na malori wasiokuwa na sifa stahiki.

Baada ya kupitia kwa kina taarifa hiyo iliyochapishwa na kusambazwa na **Allied Global Resources Limited** imebainika kuwapo kwa kipengele kinachotoa ahadi kwa waombaji hao kupatiwa cheti kutoka NIT.

Kwa kuzingatia wajibu wa kisheria wa NIT na mamlaka iliyonayo katika ithibati yake, Uongozi wa NIT unapenda kusisitiza kuwa masuala yote yanayohusu maombi ya kozi hushughulikiwa kupitia mifumo yake rasmi.

NIT inawahimiza wahusika na umma kwa ujumla kutumia njia rasmi za mawasiliano za Chuo na kupuuza chanzo chochote kinachoingilia utendaji wake.

Hatua kali za kisheria zitachukuliwa endapo taarifa hii haitasitishwa.

Imetolewa na:

Tulizo N.Chusi
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko

ALLIED
GLOBAL RESOURCES
LIMITED

# TRANSIT DRIVERS




**Je unatamani kuwa Dereva Mahiri wa Masafa Marefu ndani na Nje ya Nchi wa MABASI na MALORI lakini Huna sifa?**

FAKE NEWS

IPUUZWE

FAKE NEWS

Allied Global Resources Limited (AG... programu yake ... **Long Transit Drivers Acquisition & Skills Development ... (LT-DASS)** inakaribisha maombi kutoka kwa vijana wenye nia ... ya udereva wa mabasi na malori ya masafa marefu ...

## PROGRAMU HII INAKUPA:

- Mafunzo ya udereva wa **Masafa Marefu**
- Mafunzo ...
- Cheti kutoka ... **LATRA** Pamoja ...
- Ushauri wa Kita... na Maendeleo ya Kazi
- Ajira **NDANI** na **NJE** ya Nchi baada ya kuhitimu mafunzo

## ...BAJI:

- ...mbulisho cha Taifa **(NIDA)**
- ...na Leseni ya Udereva ya Awali inayotambulika
- Awe na Mdhamini mmoja anayefanya kazi Serikalini au ...sisi inayotambulika
- Awe tayari kuhudhuria mafunzo na kufuata masharti ya programu
- Awe na nidhamu, afya njema na utayari wa kufanya kazi za usafirishaji

**WAOMBAJI WALIOPITIA MAFUNZO YA JKT AU MGAMBO NI SIFA YA ZIADA**



**MAFUNZO YOTE YATAENDESHWA KWA UDHAMINI MAALUM**

## JINSI YA KUOMBA:

Tuma maombi yako pamoja na:

- Nakala ya Kitambulisho cha NIDA
- Nakala ya Leseni ya Udereva
- Wasifu Mfupi (CV)
- Mawasiliano ya Mdhamini

## KUPITIA:

recruitment@alliedgloballtd.com

+255 65 172 8787

USALAMA NI WAJIBU WETU

**BADILISHA MAISHA YAKO**

*Endesha Kwa Usalama, Ujenge Maisha Bora.*